**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

**SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA**

**ISO 9001:2015 Certified**

*Mwanachama wa Shirika la Viwango la Kimataifa (ISO), Codex Alimentarius Commission (WHO/FAO) na Wakala wa ISO na Mashirika ya Viwango ya Mataifa mbalimbali*

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU TAHADHARI YA USALAMA WA MAZIWA MBADALA YA WATOTO WACHANGA (BABY FORMULA) AINA YA SMA

**Dar es Salaam, 08 Januari 2026**

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linapenda kuutaarifu umma kuwa mnamo tarehe 06 Januari 2026, Kampuni ya Nestlé nchini Uholanzi (Netherlands) ilichapisha katika tovuti yake taarifa ya kusitisha na kuondoa sokoni matoleo (*batches*) kadhaa ya bidhaa ya maziwa mbadala ya watoto wachanga (*baby formula*) aina ya SMA katika soko la dunia (*recall notice*). Hatua hiyo imechukuliwa kutokana na tahadhari ya uwezekano wa kuwepo kwa sumu aina ya *Cereulide*.

Sumu ya *Cereulide* huzalishwa na vimelea vya *Bacillus cereus* na inaweza kusababisha kichefuchefu, kutapika pamoja na maumivu ya tumbo.

Aina ya maziwa hayo ya SMA yanayodhaniwa kuwa na kichafuzi hicho ni: **SMA *Advanced First Infant Milk*, SMA *Advanced Follow-On Milk*, SMA *Anti-Reflux*, SMA *Alfamino*, SMA *First Infant Milk*, SMA *Little Steps First Infant Milk*,SMA *Comfort* na SMA *Lactose Free.***

TBS inapenda kuujulisha umma kuwa matoleo (*batches*) yaliyotolewa tahadhari hayajawahi kusajiliwa hapa nchini. Hata hivyo, kutokana na hatua iliyochukuliwa na Kampuni ya Nestlé, TBS imechukua hatua za tahadhari (*precautionary measures*) kwa kuendelea kufanya ukaguzi katika soko na kuimarisha ukaguzi katika vituo vya mipakani ili kuhakikisha kuwa maziwa hayo hayaingizwi nchini.

Aidha, TBS inatoa tahadhari kwa wananchi kutonunua, kutumia au kumpatia mtoto bidhaa yoyote ya SMA ya aina zilizotajwa hadi hapo itakapotolewa taarifa rasmi nyingine. Vilevile, wananchi wanahimizwa kutoa taarifa mara moja kwa TBS endapo watakutana na bidhaa za SMA za aina zilizotajwa katika taarifa hii.

Kutokana na taarifa hiyo, TBS inawaonya waagizaji, wasambazaji na wauzaji wote wa bidhaa za maziwa mbadala ya watoto kuwa ni marufuku kuingiza, kuuza, kusambaza au kumiliki bidhaa zozote za fomula za watoto ambazo hazijasajiliwa na Shirika la Viwango Tanzania. Mtu yeyote atakayebainika kukiuka agizo hili atachukuliwa hatua kali za kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Viwango, Sura ya 130.

TBS inapenda kuuhakikishia umma kuwa itaendelea kulinda afya, usalama na maslahi ya walaji kwa kuchukua hatua stahiki bila kusita dhidi ya mtu au taasisi yoyote itakayokiuka sheria na taratibu za viwango.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali piga namba ya bure: **0800 110 827.**

Imetolewa na:

Gladness H. Kaseka

**MENEJA UHUSIANO NA MASOKO**


**TBS MAKAO MAKUU**
Shirika la Viwango Tanzania
Barabara ya Sam Nujoma / Morogoro, Ubungo, Dar es Salaam
S. L. P. 9524
DAR ES SALAAM, TANZANIA
Simu Na: +255 22 245 0298/ +255 22 245 0206
Nukushi: +255 22 2450959
Namba ya Simu Bila Malipo: 0800110827
Barua pepe: info@tbs.go.tz
Tovuti: http://www.tbs.go.tz
Barua pepe kwa ajili ya malalamiko ya wateja: malalamiko@tbs.go.tz
Twitter: TBS_Tanzania
Instagram: tbs_Viwango

**TBS KANDA YA KATI**
Jengo la Kambarage
S. L. P. 2956
DODOMA, TANZANIA
Simu Na: +255 26 2520310

**TBS KANDA YA ZIWA**
Jengo la NSSF, Ghorofa ya 3
S. L. P. 1814
MWANZA, TANZANIA
Simu Na: +255 28 2505044

**TBS KANDA YA KASKAZINI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 2399
ARUSHA, TANZANIA
Simu Na: +255 27 2520143

**TBS KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI**
Jengo la NHIF, Ghorofa ya 7
S. L. P. 1674
MBEYA, TANZANIA
Simu Na: +255 25 2502848

**TBS KANDA YA KUSINI**
Jengo la MTUWASA
S. L. P. 1396
MTWARA, TANZANIA
Simu Na: +255 23 2334477

**TBS KANDA YA MAGHARIBI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 1276
KIGOMA, TANZANIA
Simu Na: +255 28 2804023